**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Hali ya Kipindi cha Kupigania Uhuru na Mabadiliko ya Kimaudhui ya Ushairi wa Kiswahili Kati ya Miaka 1930 Hadi 1960 Nchini Tanzania

*Helina Wanjiku Njuguna[1*], Prof. Geoffrey Kitula King'ei, PhD[1] na Dkt. Richard Makhanu Wafula, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: wanjikuhelina02@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*06 Machi 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Uhuru, Ukoloni, Ushairi, Mabadiliko, Ubunifu, Maudhui, Utegemezi, Ubidhaaishaji.*

## IKISIRI

Makala hii inachunguza jinsi hali ya kipindi cha kupigania uhuru ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili kati ya miaka 1930 hadi 1960 nchini Tanzania. Kulingana na makala hii hali ni matukio mahsusi yanayoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi. Ili kukuza mjadala wetu, makala hii imezingatia kipindi cha kupigania uhuru nchini Tanganyika. Uchunguzi unazingatia mashairi teule kutoka diwani za watunzi wafuatao: Mathias Mnyampala, "Diwani ya Mnyampala (1965)", Amri Abedi, "Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri (1954)", Akilimali Snow-White, "Diwani ya Akilimali (1963)", Shaaban Robert , " Koja la Lugha (1969), Pambo la Lugha (1966), Kielezo cha Fasili (1968), na Masomo Yenye Adili (1967)", na Saadani Kandoro, "Mashairi ya Saadani, (1966)". Mashairi yaliyoteuliwa yanasomwa na kuhakikiwa ili kubainisha maudhui yaliyomo. Uchanganuzi wa data unaongozwa na mihimili ya Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha. Katika mashairi teule, inabainishwa kuwa washairi walishiriki katika siasa. Vyama vya kisiasa vilitumia Kiswahili kama chombo cha kuunganisha Watanganyika kisiasa. Mashairi yaliandikwa katika magazeti ili kuhamasisha na kuzindua watu wapiganie uhuru. Mashairi yalibeba maudhui ya dhuluma za kikoloni, utetezi wa haki, umoja wa Waafrika, uzalendo, chama cha TANU, uhuru, sifa za viongozi bora, madaraka na utamaduni wa Waafrika.

**APA CITATION**

Njuguna, H., King'ei, G. K. & Wafula, R. M. (2024). Hali ya Kipindi cha Kupigania Uhuru na Mabadiliko ya Kimaudhui ya Ushairi wa Kiswahili Kati ya Miaka 1930 Hadi 1960 Nchini Tanzania. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 124-136. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804.

**CHICAGO CITATION**

Njuguna, Helina Wanjiku, Geoffrey Kitula King'ei and Richard Makhanu Wafula. 2024. "Hali ya Kipindi cha Kupigania Uhuru na Mabadiliko ya Kimaudhui ya Ushairi wa Kiswahili Kati ya Miaka 1930 Hadi 1960 Nchini Tanzania". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 124-136. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804.

**HARVARD CITATION**

Njuguna, H., King'ei, G. K. & Wafula, R. M. (2024) "Hali ya Kipindi cha Kupigania Uhuru na Mabadiliko ya Kimaudhui ya Ushairi wa Kiswahili Kati ya Miaka 1930 Hadi 1960 Nchini Tanzania", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 124-136. doi: 10.37284/jammk.7.1.1804.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

**IEEE CITATION**

H. Njuguna, G. K. King'ei & R. M. Wafula "Hali ya Kipindi cha Kupigania Uhuru na Mabadiliko ya Kimaudhui ya Ushairi wa Kiswahili Kati ya Miaka 1930 Hadi 1960 Nchini Tanzania", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 124-136, Mar. 2024.

**MLA CITATION**

Njuguna, Helina Wanjiku, Geoffrey Kitula King'ei & Richard Makhanu Wafula. "Hali ya Kipindi cha Kupigania Uhuru na Mabadiliko ya Kimaudhui ya Ushairi wa Kiswahili Kati ya Miaka 1930 Hadi 1960 Nchini Tanzania". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Mar. 2024, pp. 124-136, doi:10.37284/jammk.7.1.1804.

## UTANGULIZI

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na umekuwa ukitumiwa kama chombo cha kuwasilishia ujumbe kwa jamii. Maudhui ya ushairi yamekuwa yakibadilika katika vipindi tofauti vya kihistoria. Baadhi ya ushairi wa urasimi mkongwe ni *Utenzi wa Al-Inkishafi (1810-1820), Utenzi wa Mwana Kupona* (1858) na *Mashairi ya Muyaka (1776-1840)* (Kezilahabi, 1983, uk.148). Maudhui ya ushairi huu yanahusu mafunzo ya kidini, wosia, siasa, na uongozi miongoni mwa mengine. Maudhui haya yalibadilika katika vipindi tofauti vilivyofuatia urasimi mkongwe kwa sababu fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo kwa wakati wake (King'ei na Kemoli, 2001, uk.4). Kwa hivyo, washairi wanaathiriwa na nguvu za mabadiliko ndani na nje ya mazingira yao.

Kati ya mwaka 1885 na 1945, kulikuwepo na vita vya dunia mara mbili. Huu ndio muhula wa utasa katika fasihi ya Kiswahili kwa sababu ya uhaba wa utunzi (Wafula na Njogu, 2007: 49). Hata hivyo, ushairi uliotungwa ukiwemo *Utenzi wa Vita vya Majimaji* na *Utenzi wa Vita vya Uhuru* (Kezilahabi, 1983, uk.149) ulikuwa na maudhui yanayohusu vita, dhuluma na ukoloni tofauti na maudhui ya ushairi wa kipindi cha urasimi mkongwe.

Katika kipindi cha urasimi mpya kuanzia mwaka wa 1945 hadi 1960, watunzi wa mashairi walianza kuchimbua miundo ya mashairi ya Ali Koti na Muyaka na kuyatumia kuyatungia yao wenyewe (Wafula na Njogu, 2007, uk.49). Kwa hivyo, walizivumbua upya kunga za utunzi na kuzitumia katika utunzi wao. Huu ndio wakati wa washairi kama Amri Abedi, Shaaban Robert, Mathias Mnyampala, Akilimali Snow- White, Khamis Amani, Saadani Kandoro na wengine. Hiki ni kipindi cha ukoloni ambapo maudhui ya ushairi wa Kiswahili yalibadilika. Katika kipindi hiki mashairi yalichapishwa katika magazeti na washairi waliteua maudhui yao kutokana na uhalisi wa maisha ya wakati ule (Mbaabu, 1985, uk.61). Ushairi ulitumika kuleta mwamko wa kisiasa na kuendeleza lugha ya Kiswahili iliyotumika katika juhudi za ukombozi (Chiragdin na Mnyampala, 1977, uk.70).

Makala hii inalenga kuchunguza jinsi hali ya kipindi cha kupigania uhuru ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili kati ya miaka 1930 hadi 1960 nchini Tanzania. Athari za kipindi hiki cha kupigania uhuru zinadhihirika katika ubunifu wa maudhui ya ushairi wa kipindi cha ukoloni.

## MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu umezingatia mihimili ya Nadharia ya Utegemezi kama inavyoelezewa na Ngugi wa Thiong'o katika kitabu chake *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature (1986)* na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha kama anavyoeleza Pierre Bourdieu katika kitabu chake *Language and Symbolic Power* (1991). Mihimili ya Nadharia ya Utegemezi inayohusu jinsi ya kusitisha hali ya utegemezi ndio iliyozingatiwa. Mhimili unaoeleza kuwa ukoloni unahusu kuharibu ama kutothamini kimakusudi utamaduni wa jamii ya Kiafrika ulizingatiwa. Mhimili huu ulitumika kuchunguza jinsi hali ya utegemezi iliweza kuondolewa kwa kupinga dhuluma za kikoloni na kutetea haki za Watanganyika.Tulichunguza jinsi washairi walivyohimiza Watanganyika waungane kupitia chama cha TANU ili kukuza umoja na uzalendo katika harakati za ukombozi. Aidha, mhimili unaoeleza kuwa jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha yao ya kienyeji kuunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

ulizingatiwa. Mhimili huu ulitumika kuchunguza jinsi ushairi wa Kiswahili ulitumika katika harakati za ukombozi. Pia, mhimili unaoeleza kuwa ili kuondoa utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha uchumi, siasa, utamaduni, lugha na waandishi wazalendo wa Afrika ulizingatiwa. Mhimili huu ulitumika kuchunguza jinsi washairi walivyotetea utamaduni, siasa na kutukuza viongozi wa Afrika katika mashairi yao.

Mhimili wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha uliotumika unaeleza kuwa watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya “soko’ yaani hadhira inayokusudiwa. Mhimili huu ulitumika kuchunguza maudhui ya mashairi ili kudhihirisha umuhimu wa lugha kama bidhaa inayouzwa sokoni. Pia, mhimili unaoeleza kuwa lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Mhimili huu ulitumika kuchunguza mchango wa mashairi katika kuenea kwa Kiswahili kwa kushughulikia masuala mbalimbali ya kijamii na kisiasa.

**Mbinu za Utafiti**

Mbinu inayotumika ni utafiti wa maktabani. Data inayotumika inakusanywa kutoka diwani nane za mashairi: *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*(1954), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Akilimali* (1963), *Koja la Lugha* (1969), *Pambo la lugha* (1966), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Masomo Yenye adili* (1967) *na Mashairi ya Saadani* (1966). Uteuzi wa diwani hizo ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio kwa kuwa na maudhui yanayozingatiwa zikilinganishwa na diwani zingine. Pia, mbinu kusudio inatumika kuteua watunzi wa mashairi kutoka katika mazingira sawa na waliotunga katika kipindi kimoja cha ukoloni. Kwa hivyo, uteuzi wao wa maudhui umeathiriwa na mazingira sawa. Usampulishaji kusudio unatumika ili kupata data kwa kuzingatia lengo la utafiti. Mashairi yaliyoteuliwa ni yale yanayobeba maudhui yanayozingatiwa bali mengine yanapuuzwa kwa kuwa hayahusiani na lengo la utafiti. Mashairi yaliyoteuliwa yanasomwa na kuhakikiwa ili kubainisha maudhui yaliyomo. Maudhui yaliyozingatiwa yanahusu dhuluma za kikoloni, utetezi wa haki, umoja na ushirikiano wa Waafrika, utamaduni wa Waafrika, sifa za viongozi bora, uzalendo, chama cha TANU, madaraka ya kujitawala, sifa kwa kiongozi Nyerere na hamu ya kupata uhuru. Uhakiki wa maudhui unaongozwa na mihimili ya Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha. Matokeo ya utafiti yanawasilishwa kwa njia ya maelezo.

**VYAMA VYA KISIASA**

Waingereza walipokuwa wanatawala nchi ya Tanganyika kuanzia mwaka wa 1918, Waafrika walilalamikia ubaguzi, mishahara duni, hali duni za maisha na kazi za lazima kutoka kwa watawala. Waafrika waliunda Chama cha Wafanyakazi wa Serikali (Tanganyika Territory African Civil Servants Association - TTACSA) mjini Tanga katika mwaka wa 1922. Kwa mujibu wa Chachage (2003) chama hiki kilidai malipo bora ya wafanyakazi, bei bora za bidhaa za kilimo na maendeleo katika kilimo. Hata katika mwaka wa 1924 Chama cha Wakulima cha Kilimanjaro yaani Native Planters Association (KNPA) kilibuniwa. Katika mwaka wa 1929 chama cha TTACSA kilianzisha chama cha kisiasa cha Tanganyika African Association (TAA). Chama cha TAA kililenga kutafuta ajira bora kwa Waafrika na kuunganisha mashirika yote ya kupigania uwakilishi wa Waafrika katika Legco (Legislative Council). Katika mwaka wa 1945 Julius Nyerere alijiunga na TAA na katika mwaka wa 1953 alichaguliwa kuwa rais wa chama. Chama cha TAA kililenga kutafuta uhuru wa kujitawala. Katika tarehe saba mwezi wa Julai mwaka wa 1954 kwenye mkutano uliokuwa Dar es Salaam, mabadiliko makubwa yalifanyiwa chama cha TAA na jina lake likabadilishwa na kuwa Tanganyika African National Union - TANU ( Were na Wilson, 1968, uk.257). Nyerere alichaguliwa kuwa rais wa chama cha TANU na Oscar Kambona akawa mhazili mkuu. Walowezi walianzisha chama cha United Tanganyika Party (UTP) katika mwaka wa 1958 ili kupinga juhudi za TANU lakini hawakufanikiwa (Chachage, 2003).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

**Matumizi ya Kiswahili Katika Vyama vya Kisiasa**

Katika Tanganyika shughuli za siasa zilipoanza kupamba moto, zilianza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano (Massamba na wengine, 1999, uk.22). Kiswahili kilikuwa silaha kubwa na muhimu kwani kilihusishwa na umoja, uhuru na uzalendo (Massamba, 1995, uk.5). Chama cha siasa kilichotangulia TANU yaani TAA kilikuwa na katiba yake iliyoandikwa kwa Kiswahili. Pia, mikutano yote ya TAA ingeendeshwa kwa Kiswahili tu (Chiragdin na Mnyampala, 1977, uk.70).

Katika mwaka wa 1954 chama cha TANU kilichopigania uhuru kutoka kwa utawala wa Waingereza, kilitumia Kiswahili kama ugwe wa kuwaunganisha watu wa makabila tofauti (Rubagumya, 1990). Mawasiliano kati ya maofisa wa chama cha TANU na watu wa mashinani hasa wale ambao walizungumza lugha za kienyeji yalitumia Kiswahili (Bienen, 1970, uk.43). Ujuzi wa Kiswahili ulikuwa jambo la lazima kwa wafanyakazi wa chama cha TANU ambao waliweza kufanya kazi sehemu mbalimbali kote nchini. Nyerere pamoja na wanachama wenzake walisafiri nchi nzima wakitumia Kiswahili kuwashawishi wananchi wajiunge na harakati za kupigania uhuru. Matawi ya chama cha TANU yalifunguliwa kwanza katika maeneo ambayo wenyeji waliweza kuzungumza Kiswahili (Whiteley, 1969, uk.65). Mikutano yote ya siasa ikawa inaendeshwa kwa Kiswahili. Kulipoanzishwa Chama cha Vijana wa TANU yaani TANU Youth League, mawasiliano yakawa kwa lugha ya Kiswahili. Kutokana na dhima hiyo, lugha ya Kiswahili ikawa ndiyo alama ya umoja, uzalendo, utanganyika na uhuru. Hata wito wa chama ukawa katika Kiswahili: Uhuru na Umoja! (Massamba na wengine, 1999, uk.22). Clarke (1960, uk.137) anaongeza kuwa afisi za chama cha TANU zilianzishwa karibu katika kila kijiji na salamu ikawa ni "Uhuru na Kazi". Lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa muhimu katika soko kutokana na matumizi yake katika shughuli za kisiasa kote nchini Tanganyika.

Aidha, chama cha TANU kiliinua elimu hasa ya watu wazima kwa kuanzisha shule za chama ili kueneza matumizi ya Kiswahili. Kiswahili kilizidi kupata nguvu kwani mwaka wa 1955 kilianza kutumiwa bungeni na ilipofika mwaka wa 1960 chama cha TANU kiliazimia kuwa Kiswahili kiwe lugha ya taifa. Tokea hapo juhudi zikawa zinafanywa ili Kiswahili kitumike katika shughuli za serikali (Chiragdin na Mnyampala, 1977, uk.70).

Kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa chombo muhimu cha kuwaunganisha Watanganyika kisiasa katika harakati za kupigania uhuru. Katika kipindi hiki cha kupigania uhuru, magazeti ya Kiswahili yalichapishwa kwa mfano, gazeti la chama cha TTACSA lililoitwa *Kwetu* na lilitoka baina ya mwaka wa 1937 na 1952 (Chiragdin na Mnyampala, 1977, uk.9). Uandishi wa mashairi katika magazeti lilikuwa jambo la kawaida (Mbaabu, 1985, uk.61). Hivyo, washairi walitekeleza jukumu la kuhamasisha na kuzindua watu ili wapate nguvu mpya za mapambano dhidi ya udhalimu wa mkoloni.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha yao ya kienyeji kuwaunganisha watu ili kuleta umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa Watanganyika ndiposa ikapata kuenea kote nchini.

## USHAIRI KAMA CHOMBO CHA KISIASA

Uhusiano kati ya ushairi wa Kiswahili na siasa ulianza zamani. Uhusiano huo unaweza kuangaliwa kwa pande mbili. Kwanza, kuna wanasiasa ambao walikuwa washairi kwa mfano, Fumo Liyongo, Zahid Mngumi, Muhammed bin Shee Mataka pamoja na washairi wa kisasa kama Amri Abedi Kaluta, Saadani Kandoro, Abdilatif Abdalla na Julius Nyerere. Pili, kuna washairi waliotunga mashairi ya kisiasa lakini hawakuwa wanasiasa. Kwa mfano, Muyaka bin Haji, Ali Koti, Shaaban Robert na Mathias Mnyampala (Mulokozi na Sengo, 1995, uk.94).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

Kulingana na King'ei na Kemoli (2001, uk.6) katika enzi za ukoloni na hata baada ya uhuru, ushairi ulitumiwa kama chombo cha kushajiisha wanajamii kuungana dhidi ya tawala za dhuluma. Washairi walitunga tungo za kishairi na wakati mwingine kwa kufumba kwa madhumuni ya kuwapinga dhulumati. Pia, Mbaabu (1985, uk.61) anashadidia maelezo hayo kwa kusema kuwa uandishi wa mashairi katika magazeti ulikuwa jambo la kawaida wakati wa ukoloni. Hizi zilikuwa ni nyakati za udhalimu wakati washairi walitumia ishara kwa wingi ili wakoloni wasielewe ujumbe wao. Huu ulikuwa wakati wa washairi kama Shaaban Robert na Saadani Kandoro.

Shaaban Robert alikuwa mshairi aliyeishi nyakati za ukoloni hivyo, hangeweza kukwepa uhalisi wa maisha ya kikoloni. Alijishughulisha na masuala ya kisiasa ya kutetea haki na kupinga unyonyaji, unyanyasaji, ubaguzi wa rangi na uovu mwingine wote (Senkoro, 1988, uk.106). Hivyo, siasa haikuachana na mashairi ya Shaaban Robert.

Kwa upande mwingine, Saadani Kandoro alijishughulisha na siasa. Kwa mujibu wa Senkoro (1988, uk.53), Kandoro alikuwa mmoja kati ya watu waliokazania sana uhuru kwa njia mbili: kimatendo na kimaandishi. Kwa upande wa maandishi Kandoro anasifika kwa ujasiri wa kuandika mashairi yaliyokashifu serikali ya mkoloni wakati ambapo mkoloni alikuwa bado nchini anatawala. Ni watu wachache walioonyesha ujasiri huu wa kumpinga mkoloni.

Kulingana na Mulokozi na Sengo (1995, uk.79) washairi wengi wa wakati wa ukoloni walioandika mashairi ya kisiasa walikuwa wanasiasa. Walikuwa viongozi wa vyama vya kisiasa vilivyopigania uhuru wa Tanganyika. Kwa mfano, Kandoro alikuwa kiongozi wa chama cha TANU mjini Tabora na Mwanza na Akilimali Snow-White alikuwa kiongozi wa Ujiji. Vilevile, Amri Abedi Kaluta alikutana na Julius Nyerere kabla ya uhuru na akamsaidia kuunda chama cha TANU, chama ambacho kilikuja kuwa cha kitaifa (Knappert, 1979, uk.284). Washairi wa kipindi cha kupigania uhuru wa Tanganyika kati ya mwaka 1950 hadi 1960 walizingatia maudhui mbalimbali kama yalivyojadiliwa.

**Dhuluma za Kikoloni**

Katika kipindi cha ukoloni kati ya mwaka 1950 hadi 1960, wakoloni waliwanyanyasa Watanganyika. Washairi walimulika unyanyasaji huo katika ushairi. Kandoro (1966, uk.146) anaeleza jinsi wakoloni walivyowanyanyasa Waafrika katika kipindi cha utawala wa Waingereza. Katika shairi "Tumshukuru Manani" anasema kuwa alifurahi sana walipopata uhuru kwani walikuwa utumwani. Mkoloni aliunda sheria ambazo hazikuwa na maana. Waafrika walibaguliwa na kutishwa kuwa wangefungwa gerezani ikiwa wangelalamika kwa kufanyizwa kazi kama punda. Waliokuwa kifungoni walipewa chakula kidogo kama vile ndege anavyotiliwa mtama kifungoni (Kandoro, 1966, uk.146). Vilevile, walilazimishwa kulipa kodi la sivyo wangefungwa kamba shingoni na kupitishwa mitaani. Aidha, hawakuruhusiwa kusoma shuleni ili waendelee kuwa wajinga. Hata pesa wasingepata wasije wakawa matajiri. Matatizo haya yote yanadhihirisha kuwa Waafrika waliteseka katika kipindi cha ukoloni.

Akilimali (1963, uk.47) anaeleza dhuluma alizopata kutoka kwa wakoloni katika shairi "Nafingwa Ningali Hai". Mshairi anatamani kueleza anayoyapitia lakini haruhusiwi kusema. Anazungumzia ubaguzi wa rangi unaomfanya akose anachotaka na sheria ambazo hazifuatwi kwa hivyo, hawawezi pata maendeleo. Aidha, ingawa ana uwezo wa kuwa kiongozi, anazuiwa asifanikiwe. Anatishwa asije akasema yale anayoyapitia kwa kupigwa magoti na kulemazwa miguu. Anasisitiza kuwa ingawa yuko hai anazibwa mdomo asiweze kusema anayoyapitia.

Pia, katika shairi "Walimwengu Tutendeje?" Kandoro (1963, uk.71) anaeleza shida zilizoingia nchini na hawajui watafanya nini. Anasema kuwa nchi yao imepata shida ingawa wanatia bidii sana shida zinawazidi kwani wananchi wanasononeka kwa sababu miradi yao imeharibika. Kwa hivyo, anaomba ushauri kuhusu shida waliyoipata. Shida iliyoko ni kulipa kodi jambo linaloathiri miradi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

yao. Wanapotaka kupanda miche mashambani nguruwe wanawawinda kwa kuwa ni maadui wao. Wanapata shida pale nguruwe wanawashinda nguvu. Hapa mshairi anafananisha wakoloni na nguruwe wanaozuia wananchi kuleta maendeleo kwa kuwadhulumu.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumika kulingana na mahitaji ya kijamii au "soko" yaani hadhira inayokusudiwa. Kwa hivyo, washairi walitumia lugha ya Kiswahili kuelezea dhuluma za kikoloni kwa lengo la kuwahamasisha Watanganyika kupigania ukombozi.

Mnyampala (1965, uk.149) anaeleza jinsi siasa zilivyokuwa wakati wa mkoloni. Katika shairi "Zama Zetu za Siasa" analinganisha jinsi siasa ilivyokuwa wakati wa ukoloni na wakati wa sasa. Anasema kwamba nyakati za zamani zimepita ambapo watu walinyanyaswa kwa vile wakoloni walijitajirisha kwa kuwanyang'anya watu pesa kwa kuwatafutia makosa. Zilikuwa nyakati zenye visa na mikasa zilizojaa dhuluma. Aidha, katika shairi "Uhuru Una Kiungo" Mnyampala (1965, uk.143) anasisitiza kuwa uhuru una kipengele kinachofuta kodi inayolipwa na wanyonge. Anawashauri watu walime wapate fedha kwani wamefanyiwa mipango. Tena wapeleke watoto shuleni wakasome hadi kiwango cha juu. Maelezo haya yanaonyesha kuwa Watanganyika walilazimishwa kulipa kodi, hawakupata faida kutokana na kilimo na walinyimwa elimu na utawala wa mkoloni.

Shaaban Robert (1967, uk.16) amekashifu ubaguzi wa rangi uliofanywa na wakoloni dhidi ya Waafrika. Katika shairi "Rangi Zetu" anasema kuwa rangi ni pambo la binadamu alilopewa na Mungu lakini si alama ya maafa. Rangi si alama ya uchafu wala si ishara ya machungu, dhambi au upungufu bali ni sifa au urembo kutoka kwa Mungu. Anasema kubagua watu kwa misingi ya rangi huonyesha upungufu kwa kuwa inaonyesha sifa ya Mungu. Mshairi anadhihirisha kuwa kudharau na kuonea wivu kwa sababu ya rangi ni upuzi wa mtu. Mshairi alilenga kukashifu ubaguzi wa rangi uliofanywa na wakoloni kwa Waafrika. Isitoshe, katika shairi "Kuondoana Njiani" Shaaban Robert (1968, uk.86) anatetea usawa kwa kupinga ubaguzi. Anasema kazi ni nyingi wanazofanya lakini hazina faida. Anabainisha dhuluma wanazopata Waafrika wanaowafanyia kazi wakoloni. Wanafanya kazi nyingi isiyo na malipo na wananyimwa haki za wanyakazi kama kuongezwa mshahara baada ya wakati fulani.

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha inasisitiza kuwa lugha hutumika kulingana na mahitaji ya kijamii inayokusudiwa. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kuelezea madhila yaliyowakumba Watanganyika wakati wa ukoloni kwa lengo la kuwahamasisha kupigania uhuru wao. Matumizi ya Kiswahili katika ushairi yalieneza lugha ya Kiswahili.

**Utetezi wa Haki**

Mnyampala (1965, uk.43) anatetea haki za wafanyakazi. Katika shairi "Watumishi Tusimame" Chama cha Wafanyikazi kinahimizwa kudai haki kutoka kwa matajiri ambao ni wakoloni. Anawashauri watumishi wa wakoloni wadai haki kila wakati yaani "jioni alfajiri" bila hasira au kupigana kwa sime. Pia, wafanyakazi wasiwe na kiburi lakini wasimame kama wanaume. Anawahimiza Waafrika waendelee na mapambano ya kutafuta haki za wafanyakazi.

Shaaban Robert (1968, uk.48) anahimiza watu waingie vitani wapambane na wakoloni. Katika shairi "Kufua Moyo" anasema kuwa siku panga itakapochomolewa mashujaa wataenda vitani na kusababisha machafuko. Ardhi italowa kwa mmiminiko wa damu. Hii ndio siku watu mashuhuri watajipambanua kwa matendo. Watu watajikusanya pamoja na kujiuliza kama ni bora kufa kwa vita au kufa kwa maradhi ya sondo. Anaendelea kusema kuwa uvundo wa maiti ya mashujaa ni sawasawa na manukato au marashi au harufu nzuri ya maua katika pua za watu. Angependa Waafrika wapambane na watawala wa kikoloni ndiposa akasema bora kufa kwa vita. Anasifu mashujaa wa kiafrika kwa kusema kuwa hata uvundo wa maiti zao ni manukato kwa watu kumaanisha wasiogope kufia vitani. Aidha, anawatia shime kwa kuonyesha kuwa hawatawahi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

kusahaulika kwa kujitolea kwao katika mapambano.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Mshairi ametumia lugha ya Kiswahili kuwahimiza Watanganyika watetee haki zao.

Kwa kuelezea sifa za ushujaa, Kandoro (1966, uk.66) anawatia moyo Waafrika watetee haki zao. Katika shairi "Shujaa Haogopi Kitu Kilicho Chake" anasema kwamba shujaa hakubali kudhulumiwa na kunyang'anywa kitu chake. Yeye haogopi kutetea halali yake. Shujaa ni hodari wa kutafuta haki yake kwa hivyo, haogopi. Anawahimiza Waafrika watetee nchi yao bila kuogopa. Pia, Waafrika wasiruhusu wakoloni kuharibu nchi au kuteka nyara miji yao lakini wafanye vyovyote vile kulinda nchi yao. Isitoshe, katika shairi "Ondoka Nchini Mwetu" Kandoro (1966, uk.141) anadhihirisha hisia zake kuhusu utawala wa Mwingereza nchini Tanganyika na Afrika kwa jumla. Anasema kuwa raia wa Tanganyika wameungana ili walinde taifa lao na waweze kujitawala. Anasema kuwa wanachama wa Chama cha TANU wanawaomba Waingereza waondoke nchini Tanganyika. Pia, Waafrika wote wameungana na kuwaomba Waingereza watoke Afrika. Anawahamasisha Waafrika wakatae utawala wa Mwingereza kwa kusisitiza kuwa Waingereza wanastahili waondoke nchini Tanganyika.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa kama bidhaa muhimu kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii na mikakati yao ya kuendeleza maisha. Lugha ya Kiswahili ilikuwa muhimu kwa sababu ilitumika kuwahamasisha Watanganyika waungane na watetee haki zao. Kwa hivyo, Kiswahili kilienea kote nchini Tanganyika.

Vilevile, katika shairi "Kujitawala" Kandoro (1966, uk.148) anawahimiza wananchi wavumilie mpaka waweze kujitawala kwani kupata uhuru si jambo rahisi. Ikiwa wanataka kujitawala inabidi wajitolee kabisa lakini si kuishi maisha ya raha. Anawaomba watu wasaidiane ili chama cha TANU kiheshimike na waungane waombe wapate kujitawala. Wakifanya hivyo, Tanganyika itatukuka duniani kote. Ana matumaini kwamba wakiomba uhuru kwa Waingereza watapata.

**Umoja na Ushirikiano wa Waafrika**

Akisisitiza umuhimu wa Watanganyika kuungana ili kupambana na mkoloni, Shaaban Robert (1966, uk.9) anasema katika shairi lake "Chama cha Waafrika" kuwa baada ya kuwaza amegundua upekee hauna faida hasa wakati wa shida. Hivyo, ikiwa wananchi wanataka kujitawala lazima washirikiane. Wananchi wanastahili kujiunga na Chama cha Waafrika cha Watanganyika kwa sababu ni shirika linalotukuka linalonuia kuzuia mateso kwa wananchi. Chama pia kinaeleza serikali ya Waingereza shida wanazopitia wananchi. Mshairi anawahimiza wananchi waungane kwa sauti moja ili Waingereza wajue kuwa wanawaumiza. Pia, anawahimiza Watanganyika waungane katika harakati za ukombozi.

Nadharia ya Utegemezi inasisitiza kuwa jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Lugha ya Kiswahili ilitumika kuwahimiza Watanganyika na Waafrika kwa jumla washirikiane katika harakati za ukombozi. Hivyo, kupitia mashairi, lugha ya Kiswahili ilienea.

Kwa upande mwingine, Mnyampala (1965, uk.147) anawashauri watu waungane waweze kupambana na wakoloni. Katika shairi"Muungano Utupambe" mshairi anamwomba Mungu awaondolee mizozo ili mataifa yasigombane. Anasisitiza kuwa viumbe wote wanastahili waungane pamoja, waondoe ugomvi na machukizo ili waishi kwa amani. Analenga kuwahimiza Waafrika washirikiane popote walipo ili wakabiliane na matatizo yao. Isitoshe, katika shairi "Shirika ni Kustawi" Mnyampala (1965, uk.23) anasisitiza kuwa ushirikiano huleta mafanikio na kufarakana ni vibaya. Anasema anayeacha wengi ni mchawi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

kwa sababu shirika ni nzuri. Ni wazimu kuharibu upendo kwa kuchomana kama takataka kwani mapenzi yakiwepo shirika linadumu na watu huishi kwa furaha. Katika shairi hili mshairi anabainisha umuhimu wa ushirikiano katika jamii.

**Kupigania Utamaduni wa Waafrika**

Amri Abedi (1954, uk.52) anapigania utamaduni wa kiafrika kwa kukashifu tabia ya wanawake wa Afrika ya kuvaa mavazi ya kigeni katika shairi lake "Nguo Ziteremsheni Yapungue Maasia." Anasema kuwa ni heshima kuvaa nguo ndefu hadi miguuni. Wanawake wasiige mavazi ya wengine kwani nguo baya ni baya hata kama imetoka uzunguni. Anadhamiria kuonya wanawake dhidi ya kuiga tabia za kigeni kama vile kuvaa nguo fupi zinazowafedhehesha na kuwadunisha mbele ya macho ya umma. Anasema "baya ni baya tambua ingawa la uzunguni" kuonyesha kuwa uvaaji wa nguo fupi si utamaduni wa Waafrika bali ni wa Wazungu.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha utamaduni wao ili kuondoa utegemezi. Watunzi wa mashairi walihimiza Watanganyika wadumishe utamaduni wao kwa kukashifu utamaduni wa Kizungu hasa unaohusu mavazi.

Aidha, katika shairi "Wakudao Magotini Hawachelei Khasar" Abedi (1954, uk.53) anaendelea kukashifu tabia ya wanawake ya kuvaa nguo fupi. Anashangaa jinsi buibui na kanga ndefu hupandishwa magotini na ni nguo za heshima. Anasema kuwa wanaoiga tabia za Wazungu bila kufikiria ni wajinga. Anatetea utamaduni wa Waafrika kwa kuwaonya wanawake wa Afrika wasiige tabia za Wazungu zinazohusiana na mavazi kwani wanajikosesha heshima na kusababisha maovu mengi. Isitoshe, katika shairi "Njema Haina Mkosi Japo aivae Koja" Abedi (1954, uk.55) anaendelea kukashifu wanawake wanaovaa nguo fupi. Anasisitiza kuwa Wahindi wakivaa nguo fupi huwa ni njema kwao lakini ni balaa kwa Waafrika. Anasema wanawake kuvaa nguo fupi ni ujinga na ushetani. Shairi hili linatetea utamaduni wa Mwafrika kwani mshairi anaonya wanawake wa Afrika wasiige mavazi ya Wahindi hata kama ni mazuri kwa Wahindi.

**Sifa za Viongozi Bora**

Suala la uongozi limeshughulikiwa na Akilimali (1963, uk.29). Katika shairi "Manahodha Kuwa Wengi" mshairi anaelezea sifa za viongozi bora. Anasema kuwa ingawa kiongozi amesoma na kuihitimu mitihani ya Ulaya, lakini akiwa mkaidi au mpinzani, nchi haitaendelea ndiposa akasema "meli haitaelea". Shairi hili linadhihirisha umuhimu wa kiongozi bora kwa sababu huleta maendeleo nchini. Aidha, katika shairi "Kila Mpenda Rushuwa" Akilimali (1963, uk.23) anawaonya viongozi dhidi ya kuchukua hongo kwani itawatia jela. Anasema kuwa tamaa nyingi ya pesa ni hatari kwani itamtia mtu jela. Hivyo, analenga kuwaonya viongozi yaani "wenye vyeo" kama vile mahakimu wajihadhari kwani rushwa itawatia gerezani. Vilevile, mshairi anawaonya wanaotaka hadhi au utukufu kwa njia isiyo halali kuwa watapatwa na maafa. Pia, katika shairi "Kila Mtaka Uluwa" Akilimali (1963, uk.19) anasema kuwa mtu anayetaka cheo kwa kasi hujitia kwenye matatizo kwa sababu hawezi kukaa na kutulia bali hujitia hatiani. Anashauri kuwa kutafuta vyeo hakuhitaji nguvu, vishindo au ghasia bali kunataka uvumilivu. Mshairi analenga kuwashauri wanaotaka uongozi kwamba watumie njia halali na wanapokosa vyeo hivyo wakubali wameshindwa.

Kwa upande wake, Shaaban Robert (1968, uk.37) anaangazia suala la uongozi katika shairi lake "Kashata na Ladu". Mshairi analinganisha serikali za wanyama, ndege, na wadudu na serikali za watu. Anasema kuwa wanyama, ndege na wadudu wana serikali zilizo na fahari iliyo kama ibada ya dini lakini watu wenye busara hawawezi kuchukua madaraka na kuheshimika kuliko wanyama na wadudu. Anaonyesha kuwa viongozi huendeleza dhuluma na kuangamiza watu. Hivyo, watu hawawezi kuwaheshimu kwa sababu wanafurahia uadui.Tena, katika shairi "Kosa Ndogo" Shaaban Robert (1968, uk.50) anaonyesha athari za makosa ya viongozi. Anasema kuwa ni jambo lisilo la maana kutangaza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

habari ya kosa la mtu mdogo au wa kawaida kwa sababu tendo lake ni kama la mwendawazimu ambalo wenye akili timamu hawawezi kulipatiliza. Makosa makubwa hufanywa na viongozi ingawa hufichwa kwa uangalifu mkubwa. Kwa hivyo, walimwengu hutukuza wahalifu wakubwa na kuaibisha maskini.Viongozi huwadhulumu maskini ili wafaidi cha maskini lakini hawafanywi chochote kwani maskini hawana uwezo wa kutenda lolote. Anabainisha maonevu kwa wanyonge. Viongozi wanawadhulumu wanyonge lakini wanatukuzwa ila wanyonge wanaoneshwa kuwa ndio wenye kosa.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa lugha, lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Lugha ya Kiswahili ilitumiwa kuelezea sifa za viongozi bora huku ikikashifu viongozi wabaya. Matokeo yake ni kuwa lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini Tanganyika.

**Uzalendo**

Suala la uzalendo limeshughulikiwa na Akilimali (1963, uk. 19). Katika shairi "Kila Ndege na Tundule" mshairi anatumia jazanda ya ndege kuashiria mwenyeji wa lugha fulani na tundu kurejelea lugha asilia. Anasema hata lugha iwe nzuri namna gani lakini ni ya kigeni, haiwezi ikampendeza mtu aliye na lugha yake asilia. Anadhihirisha mapenzi yake kwa lugha ya Kiswahili; lugha yake ya asili. Pia, katika shairi "Kila Mdharau Chake" Akilimali (1963, uk.21) anaonya anayedharau lugha yake kwani ataangamia. Amelaaniwa kwa kukidharau, kukikana na kukitupa kilicho chake na kupendelea cha mwingine. Mshairi anarejelea anayedharau lugha yake ya asili hasa Kiswahili. Mwenyeji anastahili aitunze, ainene na aipe hadhi lugha yake. Anaisifu na kuitetea lugha yake ya Kiswahili ili idumishwe na kupewa hadhi yake. Aidha, katika shairi "Kiswahili" mshairi anaendelea kuisifu lugha ya Kiswahili. Anasema kuwa Kiswahili ni lugha yake ya asili aliyoizungumza tangu utotoni hadi utu uzima. Anajieleza vizuri bila hofu kwa kuwa ana ufasaha wa lugha. Anasema kwamba ingawa anajitahidi kujifunza na kusoma lugha za nchi zingine, hafanikiwi. Anaisifu lugha ya Kiswahili kwa kuilinganisha na lugha zingine.

Nadharia ya Utegemezi inasisitiza kuwa ukoloni unahusu kuharibu ama kutothamini kimakusudi utamaduni wa jamii. Washairi walisitisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kuthamini na kutukuza lugha ya Kiswahili katika kazi zao.

Kwa upande mwingine, Shaaban Robert (1966, uk.27) anashadidia maoni ya Akilimali ya kuisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili. Katika shairi lake "Kiswahili" anatumia sitiari ya "titi la mama" kubainisha utamu na uzuri wa Kiswahili tofauti na lugha nyingine. Anasema kuwa Kiswahili ni lugha yake tangu utotoni hadi utu uzima. Ni lugha anayoipenda ndiposa akaifananisha na manukato yanayopendeza. Anaitumia popote anapopitia kwa sababu ni tamu kuliko lugha nyingine. Mshairi anaisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili huku akidhihirisha umuhimu wake katika jamii.

Suala la uzalendo limeshughulikiwa pia na Mnyampala (1965, uk.127). Katika shairi lake "Lugha Yetu Kiswahili" anaisifu lugha ya Kiswahili. Anasema kuwa ataisifu na kujivunia lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni lugha njema katika mawasiliano hasa kwa wageni tena inatumiwa shuleni, bungeni na katika biashara. Pia, Kiswahili hutumika kama lugha ya kufundishia masomo ya kiufundi na katika dini hasa kwa kusali. Kwa hivyo, Kiswahili ni lugha yenye majukumu mengi katika jamii.

Fauka ya hayo, Mnyampala (1965, uk.154) anaendelea kusifu lugha ya Kiswahili katika shairi "Kimefuzu Kiswahili". Anaeleza furaha aliyonayo kwa Kiswahili kuteuliwa kitumike katika Baraza kuu. Anapendekeza Kiswahili kitunzwe na kiombewe kiweze kuenea kote nchini. Anasema kuwa lugha nyingine hazifai kwani hawawezi kujieleza vilivyo hata wanapotosha kauli kwa kutozijua vyema. Katika shairi hili mshairi anaisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

utamaduni na lugha yao ili kuondoa utegemezi wa lugha za kikoloni. Watunzi wa mashairi walitetea lugha ya Kiswahili kwa kuisifu na kuitukuza huku wakisitisha utegemezi wa lugha za kikoloni katika mawasiliano. Jambo hili lilieneza lugha ya Kiswahili kote nchini.

Amri Abedi (1954, uk.98) ameshughulikia suala la uzalendo kupitia shairi lake "Uhuru jambo Halisi". Katika shairi hili anadhihirisha mapenzi kwa nchi yake inayotawaliwa na mkoloni anayewanyima uhuru. Anasema nchi ikiwa nzuri lakini wananchi wakose uhuru huwa na taabu sana. Anakiri kuwa anaipenda nchi yake kwa sababu ana haki ya kuishi. Anawaomba Watanganyika waungane waweze kupigania uhuru. Ana matumaini kuwa siku moja watakuwa huru. Mshairi anadhihirisha uzalendo kwa nchi yake kwa kuwa tayari kuipigania ipate uhuru.

Uzalendo kwa taifa ni suala linaangaziwa na Akilimali (1963, uk.83) katika shairi lake "Lipende Taifa Lako". Mshairi anasema kuwa mtu anapopenda taifa lake kwa dhati na kuisherehekea, hata yeye anasifika kwa kuwa mzuri. Anashauri mtu apende taifa na kisha alitumikie. Anawashauri watu wasiogope kifo kwa ajili ya taifa na wazingatie umoja. Anatahadharisha wasikubali kukashifu taifa lao hata wakipigwa au kubadili taifa kwa mali heri hata wafe. Mshairi anawahimiza watu wapende taifa lao na kujitolea kulipigania na kulitumikia.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya jamii iliyokusudiwa. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kubainisha umuhimu wa uzalendo kwa taifa la Tanganyika. Hivyo, kupitia kwa ushairi lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini.

## Mchango wa Chama cha TANU katika Kuunganisha Wananchi

Kandoro alikuwa mmoja wa watu kumi na saba walioanzisha chama cha TANU (Kandoro 1966, uk.146). Hivyo, aliwahimiza Waafrika waungane ili kutetea uhuru wa Watanganyika. Katika shairi "Waafrika Njooni" Kandoro (1966, uk.139) anawaita Watanganyika wajiunge na chama cha TANU. Anawasihi wasikae ujingani lakini wafahamu chama chao ni kimoja tu na ni cha TANU. Anasema lengo kuu la chama hicho ni kuunganisha watu wa makabila tofauti ili wapiganie uhuru. Anadhihirisha umuhimu wa Watanganyika wa kujiunga na chama cha TANU ili kupigania uhuru wao.

Nadharia ya Utegemezi inasisitiza kuwa jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Lugha ya Kiswahili ilikuwa lugha ya mawasiliano katika shughuli za chama cha TANU. Ilitumika kuwahimiza Watanganyika wajiunge na chama cha TANU na washirikiane katika harakati za ukombozi. Hivyo, kupitia mashairi, lugha ya Kiswahili ilienea.

Mnyampala (1965, uk.31) anasifu chama cha TANU kutokana na ushindi wake katika uchaguzi kwenye shairi "Kura Tumezifagia". Mshairi anasema kuwa lisije likaonekana kama jambo ndogo kuwa chama cha TANU kimeshinda kwa kura tatu na kupata wawakilishi serikalini. Katika shairi hili mshairi anaonyesha mafanikio ya chama cha TANU kwa kushinda kura tatu. Pia, anabainisha matarajio yake kuwa chama cha TANU kingekuwa chombo cha kudai uhuru.

Shaaban Robert (1966, uk.9) anawaomba Watanganyika wajiunge na chama cha TANU. Katika shairi "Chama cha Waafrika" anasema kuwa watu wanapaswa waungane kama wanataka kujitawala. Kila mtu anaombwa ajiunge na Chama cha Waafrika ambacho kingetumika kuelezea wakoloni matakwa yao. Waafrika wangefanikiwa ikiwa wangekuwa na umoja katika kutetea haki zao. Mshairi anawahimiza Watanganyika wajiunge na Chama cha Waafrika ili waweze kupigania uhuru.

## Madaraka ya Kujitawala

Mnyampala (1965, uk.131) anaelezea furaha aliyokuwa nayo nchi ya Tanganyika ilipopata madaraka mwezi wa Oktoba tarehe kumi na moja. Katika shairi "Siku ya Historia" anasema kuwa Oktoba kumi na moja ni siku ya kukumbuka kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

sababu nchi yake ilikuwa imepiga hatua ikikaribia kupata uhuru. Waliitazamia siku ya kupata madaraka kama gavana alipokuwa amewaahidi. Mshairi anadhihirisha matumaini ya Watanganyika ya kupata uhuru baada ya kuwa na madaraka. Aidha, katika shairi "Ni Madaraka Kamili" Mnyampala (1965, uk.139) anasherehekea kupatikana kwa madaraka kamili. Anamshukuru Mungu kwa kuwapa uongozi wasiendelee kunyanyaswa. Anatamani mwezi wa Disemba ufike wabadili bendera ya mkoloni na kutundika ya Watanganyika kwa kupata uhuru kamili. Suala la madaraka nchini Tanganyika linaangaziwa pia katika shairi "Mpya Sasa Tanganyika". Katika shairi hili Mnyampala (1965, uk.97) anasema nchi mpya imeumbika kwa hivyo, ana haki ya kufurahi kwani ya kale yametoweka. Anahimiza majirani wa Tanganyika wakazanie siasa njema ili Mungu awajalie madaraka. Mshairi anabainisha furaha yake kwa Tanganyika kupata madaraka na kutangulia nchi zingine za Afrika Mashariki. Vilevile, katika shairi "1960 Madaraka Tumebeba" suala la madaraka limefafanuliwa. Mnyampala (1965, uk.91) anasema huu ndio mwaka wa kumpamba Nyerere kwa sababu ni kipenzi chao. Amewaongoza vyema mpaka wakapata madaraka na kilichobaki ni uhuru kamili. Alisikiliza hotuba alipokuwa Lejiko ilipotangazwa kuwa wangepewa madaraka ndipo akafurahi sana. Watanganyika walikuwa na katiba yao ambayo ingewaongoza na mambo yanayohusu dhuluma na ukiukaji wa haki yalikuwa yamefika mwisho. Mshairi anaonyesha furaha waliokuwa nayo Watanganyika kwa kupata madaraka huku wamengoja uhuru kamili.

Kwa mujibu wa Nadharia ya ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa kama bidhaa muhimu na yenye thamani kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii. Kwa kuwa ushairi wa Kiswahili ulitumiwa na Watanganyika kudhihirisha furaha yao ya kupata madaraka, Kiswahili kilienea kote nchini.

**Sifa kwa Kiongozi Nyerere**

Nyerere alikuwa kiongozi wa chama cha TANU kilichopigania uhuru nchini Tanganyika**.** Mnyampala (1965, uk.102) anamsifu na kumtakia mema. Katika shairi "Twaomba Ubarikiwe" mshairi anamwombea Nyerere na jamii yake wabarikiwe. Mshairi anaanza utungo wake kwa kulishukuru gazeti la *Kiongozi* kwa kuwafahamisha waziwazi familia ya Nyerere. Anamtaja Nyerere kama kiongozi mwenye huruma aliyetaka Watanganyika waokolewe. Katika shairi hili mshairi anaonyesha mapenzi yake kwa Nyerere kwa mchango wake nchini Tanganyika. Hivyo, anaomba Mungu ambariki pamoja na familia yake.

Nadharia ya Utegemezi inasisitiza kuwa Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha siasa zao ili kuondoa utegemezi wa utawala wa kikoloni. Washairi wa Kiswahili walimtukuza na kumsifu Nyerere kutokana na mchango wake katika harakati za kupigania ukombozi wa nchi ya Tanganyika.

Fauka ya hayo, Mnyampala (1965, uk.137) anamsifu kiongozi Nyerere katika shairi lake "Mungu Mwongoze Rubani" kwa kutumia sitiari ya rubani kuashiria kiongozi Nyerere. Anasema kuwa wanakaribia kupata uhuru licha ya matatizo waliyoyapata. Nyerere amekuwa kiongozi mwema aliyesimama imara. Watanganyika walimwamini kama kiongozi wao ambaye angeongoza safari ya kupigania uhuru mpaka ikamilike salama. Ijapokuwa walipigania uhuru hakuna mtu aliyeumia na damu haikumwagika. Mshairi anamsifu Nyerere kwa uongozi bora. Isitoshe, katika shairi "Duri Nadawiri Zari" Mnyampala (1965, uk.142) anamsifu Mheshimiwa Nyerere. Anasema kuwa siku ya uhuru tarumbeta zitavumishwa na bendera kupangwa na askari huku wananchi wakisherehekea. Pia, kiongozi Nyerere ataheshimika kwa kupambiwa taji sawa na Watemi mashuhuri. Nyerere amekumbana na matatizo mengi na kushambuliwa na maadui lakini aliweza kuwashinda. Katika shairi hili mshairi anamsifu kiongozi Nyerere kwa ushujaa na uongozi bora.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804

**Hamu ya Kupata Uhuru**

Abedi (1954, uk.98) anadhihirisha hamu ya kupata uhuru katika nchi ya Tanganyika. Katika shairi “Uhuru Jambo Halisi” anasisitiza umuhimu wa uhuru na kuukosa ni taabu. Anasema hata tundu liwe la dhahabu na lenye milango iliyotengenezwa kwa mbao za mpingo, ndege akiwa ndani na kufanywa mahabusu huiona adhabu. Mshairi anatumia jazanda ya tundu na ndege kumaanisha kuwa mtu akifanywa mahabusu katika nchi yake hukosa raha na hutaka kuwa huru. Ana matumaini kuwa kuna siku itafika wananchi wajitawale na dhiki na wasiwasi zifike mwisho. Mshairi anabainisha matatizo wanayoyapata Waafrika kama vile ubaguzi, ukiukaji wa haki na unyanyasaji. Anatamani wapate uhuru ili matatizo yao yaishe. Pia, katika shairi “Kiwakacho Huzimika” Abedi (1954, uk.103) anamwomba Mungu awajalie uhuru. Anasema kuwa ana huzuni na roho yake inataabika lakini anaamini kuwa kila jambo lina mwisho wake. Anashangazwa na jinsi wanavyodhulumiwa. Mshairi anadhihirisha hisia zake kutokana na unyanyasaji. Anamwomba Mungu awajalie uhuru ili waishi maisha mema.

Mnyampala (196, uk. 136) anadhihirisha hamu ya kupata uhuru nchini Tanganyika. Katika shairi “Mungu Zidisha Uhai” anamwomba Mungu awazidishie uhai ili waione siku ya uhuru. Anamshukuru Mungu kwa wema wake na kumwomba awaruhusu wawe na uhuru. Wanaingojea kwa hamu siku njema matumaini yao yatakapotimizwa watu wote wafurahi. Dhuluma na vitisho vitakuwa vimeisha kwa sababu watakuwa wamepata walichokipigania kwa muda. Mshairi anadhihirisha hamu ya Watanganyika ya kupata uhuru. Isitoshe, katika shairi “Uhuru Uwe wa Kheri” Mnyampala (1965, uk.144) anabainisha hamu na matumaini ya Watanganyika ya kupata uhuru. Anasisitiza kuwa angependa uhuru uwe wa kheri na udumu kwa amani. Mshairi anamwomba Mungu awaondolee unyanyasaji ili Tanganyika iwe shwari na iweze kukua na kuwa huru. Mshairi anaonyesha kuwa uhuru umepatikana ndipo akasema “uhuru umewasili, pasipokuwa na dosari” lakini wastahili udumu kwa amani.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya jamii iliyokusudiwa. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kubainisha hamu waliyokuwa nayo ya kupata uhuru wa Tanganyika. Hivyo, kupitia kwa ushairi lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini.

## HITIMISHO

Makala hii imefafanua jinsi hali ya kipindi cha kupigania uhuru ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili kati ya miaka 1930 hadi 1960 nchini Tanzania. Imebainika kuwa washairi wengi wa wakati wa ukoloni walikuwa wanasiasa walioongoza vyama vya kisiasa. Pia, kuna mashairi ya kisiasa yaliyotungwa na washairi wasiokuwa wanasiasa. Hivyo, washairi hawakujitenga kisiasa kwani kuna wale walioshiriki au kuandika kuhusu harakati za ukombozi wa Watanganyika. Vyama vya kisiasa vilitumia lugha ya Kiswahili kama chombo cha kuwaunganisha Watanganyika kisiasa. Uandishi wa mashairi katika magazeti ulikuwa jambo la kawaida ili kuhamasisha na kuzindua watu wapiganie uhuru. Lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini kutokana na majukumu yake katika jamii. Mashairi yalibeba maudhui mbalimbali yakiwemo: dhuluma za kikoloni, utetezi wa haki, umoja na ushirikiano wa Waafrika, utamaduni wa Waafrika, sifa za viongozi bora, uzalendo, chama cha TANU, madaraka ya kujitawala, sifa kwa kiongozi Nyerere na hamu ya kupata uhuru. Kwa hivyo, maudhui ya ushairi wa Kiswahili katika kipindi cha urasimi mpya yanatofautiana na ya vipindi vya urasimi mkongwe na utasa.

## MAREJELEO

Abedi, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Akilimali, K. (1963). *Diwani ya Akilimali*. Nairobi: East African Literature Bureau.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1804


Bienen, H. (1970). *Tanzania: Party Transformation and Economic Development.* Princeton, New Jersey: Princeton University Press.

Bourdieu, P. (1991). *Language and Symbolic Power*. Harvard University Press: United States

Chachage, C. (2003). Globalisation ana Democracy Governance in Tanzania. In *Development Policy Management Forum* (www). http://www.dpmf.org/publications/occassional%20papers/occasionalpaper10.pdf

Chiragdin, S., na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Clarke, P. (1960). *A Short History of Tanganyika: Mainland of Tanzania.* Tanzania: Longman.

Kandoro, S. (1966). *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing Limited.

Kezilahabi, E. (1983). Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili. *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. *Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.*

King'ei, K., na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili: A Literary History and Anthology*. London: Heinemann.

Massamba, D. Kihore, Y. na Hokororo, J. (1999). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo. *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.*

Massamba, D. P. B. (1995). Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano. *Kiswahili katika Kanda ya Afrika ya Mashariki*. *Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research*, 1-11.

Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research and Literature*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: Kenya Literature Bureau

Mulokozi, M., & Sengo, T. (1995). *History of Kiswahili Poetry A.D1000-2000: A Report.* University of Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Ngugi, T. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Robert, S. (1966). *Pambo la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.

Robert, S. (1967). *Masomo Yenye Adili*. Nairobi: Nelson.

Robert, S. (1968). *Kielezo cha Fasili*. Nairobi: Nelson.

Robert, S. (1969). *Koja la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.

Rubagumya, C. (1990). *Language in Education in Africa: A Tanzanian Perspective*. Clevedon. Philadelphia: Multilingual Matters Limited.

Senkoro, F. (1988).*Ushairi: Tahakiki na Nadharia*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Wafula, R., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Were, G., & Wilson, D. (1968). *East Africa through a Thousand Years: AD 1000 to the Present Day*. London: Evans Brothers Limited.

Whiteley, W. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.